

## HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO

Tel. 0262968010/0785261723  
 Fax: 0262968010  
 Website: www.Kilolodistrict.go.tz



S.L.P.2324,  
 KILOLO,  
 06/09/2017

## TANGAZO LA ZABUNI-(LGA/027/2017/2018/G/1-9)

Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo inakaribisha maombi ya zabuni kutoka kwa wafanyabiashara/vikundi / Taasisi mbalimbali zenye sifa na uwezo wa kununua Miti ambayo Halmashauri itauza kupitia shamba lenye umri wa **miaka 17** katika Tarafa ya Kilolo Kata ya Ukumbi kwenye **Msitu wa Masalali kuna viunga 9 vyenye jumla ya mita za ujazo 1,806.017.(m3)** Miti aina ya (**Pini-Pinus patula**) na bei elekezi imetolewa kwa kila kiunga, Pia msitu huo una miti aina ya Mikaratusi (**Eucadyptus spp**) **109** yenye kipenyo cha **sm30** na kuendelea na imwekewa alama hiyo ni zabuni inayojitegemea kwa msitu wote.Miti hiyo itauzwa ikiwa imesimama shambani kwa utaratibu wa zabuni zilizofungwa kama ilivyoelezwa katika **kanuni ya Misitu 2004 (The Forest Regulation 2004)**. Mwombaji unakaribishwa kuleta zabuni yako yenye bei kwa kila kiunga/mita za ujazo kama ilivyoelezwa

## MASHARTI YA WAOMBAJI

Mwombaji anatakiwa atimize masharti yafuatayo:

1. Awe na leseni ya biashara
2. Leseni ya usajili wa biashara ya mazao ya Misitu (Uvunaji na Uchakataji miti) kwa mwaka 2015/2016.
3. Awe amesajiliwa kama mlipa kodi (TIN)
4. Mwombaji ataje bei (OFFER) kwa kila kiunga katika Fomu ya maombi,
5. Mwombaji aandike kwenye fomu ya maombi muda atakao tumia kuvuna miti baada ya kujulishwa kuwa ameshinda zabuni na kusaini mkataba.
6. Mwombaji alipe ada ya maombi kwa kila kiunga jumla ya Tshs. **50,000/= (elfu hamsini tu)**, fedha hizo hazitarejeshwa.

## NB: Nakala ya stakabadhi ya malipo iambatanishwe na maombi

7. Maombi yafungwe kwenye bahasha vizuri , juu ya bahasha iandikwe aina ya zabuni inayoombwa bila kuonyesha alama yoyote ya sehemu maombi yanakotaka
8. Mwombaji asiwe anadaiwa na Halmashauri ya Wilaya
9. Mwombaji atakaeshinda atalazimika kulipia malipo yote ndani ya muda wa siku tano(5) kuanzia ziku ya kubandikwa tangazo la ushindi wa zabuni kwenye ubao wa matangazo wa Halmashauri/ au kupewa taarifa ya ushindi wa zabuni hiyo,
10. Mshindi wa zabuni ambae atashindwa kulipia zabuni yake ndani ya muda uliowekwa atahesabiwa kama mvurugaji wa zabuni na atachukuliwa hatua ikiwemo kutoruhusiwa kuomba tena zabuni katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo.
11. Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo itatoa mkataba kwa mzabuni ambae zabuni yake imeamuliwa kuwa inafaa na ambae ametoa zabuni ya bei ya iliyotathiminiwa kuwa ya juu. Rasimu ya mkatakaba imeambatanishwa katika kablasha la zabuni.
12. Siku ya kutembelea msitu itakua **Jumatatu tarehe 18 HADI 28-22/09/2017 kuanzia saa 3:00 asubuhi hadi saa 9.30 jioni, Safari itaanza katika ofisi ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, baada ya tarehe hiyo gharama za kutembelea msitu zitakua za mzabuni mwenyewe.**
13. Kablasha la zabuni linapatikana katika ofisi ya Katibu wa Bodi ya zabuni, Kuanzia jumatatu hadi Ijumaa saa **2:30** asubuhi hadi saa **9:30** isipokuwa siku za sikukuu na mapumziko.
14. Kwa waombaji ambao shughuli zao zinapaswa kusajiliwa na mamlaka husika watapaswa kuonesha uthibitisho wa usajili wao/vibali vya kuruhusu kufanya kazi hizo.
15. Maombi lazima yaambatanishwe na hati za kuonesha umiliki wa shughuli au kampuni nakala lazima ithibitishwe (certify) na hakimu / mwanasheria
16. Waombaji ni lazima waoneshe anwani zao kamili na mahali ofisi zao zilipo
17. Maombi hayo yatumwe kwa:

**KATIBU,  
 BODI YA ZABUNI,  
 HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO,  
 S.L.P. 2324,**

18. Maombi yatakatwa kwenye ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (w)
19. Maombi ambayo hayatazingatia masharti yaliyotajwa hapo juu hayatafikiriwa wala kushughulikiwa
20. Maombi yatakayofika baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha zabuni hayatapokelewa
21. Mwisho wa kupokea maombi ni siku ya **Jumane** tarehe **26/09/2018** saa **4:00** asubuhi na zabuni zitafunguliwa saa **4:30** Asubuhi hiyo hiyo katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya chumba **Na.19**, Hivyo wahusika na wawakilishi wa waombaji husika wanakaribishwa kuhudhulia zoezi la ufunguzi .

Tangazo hili nimetolewa na



**ALOYCE KWEZI**  
**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO**  
**KILOLO**

382160006